**PRIMARY EDUCATION SERVICES NETWORKING ORGANIZATION (PESNO)**

**SIMU: 0713- 526533**

**0767- 526533**

# MTIHANI WA KWANZA WA UTAMILIFU KWA DARASA LA SABA

## SOMO: KISWAHILI [03]

**TAREHE 8/03/2021** **MUDA: SAA 1:30**

**NAMBA YA MTAHINIWA:** ______________________________________________________

**JINA LA SHULE:** __________________________________________________________

**WILAYA**: ____________________ **MKOA:** ____________________

## MAELEKEZO:

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya majibu
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. chagua jibu sahihi kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia (OMR)kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya karatasi ya (OMR)
5. Hakikisha kazi yako iko nadhifu na safi
6. Mtihani huu una kurasa nne zilizochapishwa

## SEHEMU A: SARUFI NA LUGHA YA KIFASIHI:

1. Mgeni wa ajabu alifanikiwa kumdhuru nani?
   a. Wenyeji b. watoto c. wote d. hakumdhuru mtu e. hakumdhuru yeyote
2. Andika nahau yenye maana ya kudhihaki
   a. Fanya zihaka b. cheza shere c. piga dhiki d. cheza kindakindaki e. cheza sherehe
3. Nani hakumuelewa mgeni vizuri?
   a. Watoto b. watu wazima c. kila mtu d. mgeni e. wanawake
4. Neno mandhari kama lilivyotumika katika habari hii lina maana gani?
   a. Zingira b. muonekano wa watu wa mahali c. sura ya mahali d. vitu vya mahali e. sura ya watoto wa mahali
5. Nani alianza kumdhihaki mgeni?
   a. Watu wazima b. wazee c. hakuna aliyedhihaki d. wote e. watoto
6. Wanafunzi wa darasa la saba wanafanya mtihani. Neno mtihani limetumika kama aina gani ya maneno?
   a. Kielezi b. kitenzi c. nomino d. kivumishi e. kiwakilishi
7. Kipande cha chuma kinachopigiliwa dirishani au mlangoni ili uweze kufungwa na kufunguliwa huitwa_____________
   a. Chomeko b. bawabu c. engo d. bawaba e. shata
8. Siku ya harusi ya mjomba, watu walikunywa pombe ___________ sita
   a. Balasi b. vibalasi c. mabalasi d. mibalasi e. wabalasi
9. Mjomba Issa amenunua ng'ombe **<u>wa</u>** maziwa. Neno llilopigiwa mstari limetumika kama___
   a. Kiunganishi b. kishirikishi c. kivumishi d. kihusishi e. kielezi
10. Katika maneno yafuatayo neno lipi lina maana sawa na neno posho
    a. Kifungua kinywa b. ajira c. mshahara d. motisha e. tija
11. Wanakijiji wa Pawaga watachagua viongozi wa kijiji chao mapema. Sentensi hii ipo katika wakati gani?
    a. Uliopo b. unaoendelea c. ujao d. uliopita e. mtimilifu
12. Neno lipi halihusiani na mengine kati ya maneno yafuatayo?
    a. Uchunguzi b. udadisi c. uchochezi d. upekuzi e. upelelezi
13. Pale _____ alipoingia mkuu wa wilaya. Neno lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?
    a. Ndiyo b. ndilo c. ndimo d. ndipo e. ndiye
14. Mahali wanapowekwa watuhumiwa wakisubiri kesi zao kusikilizwa huitwa___
    a. Gerezani b. jela c. ndani d. polisi e. mahabusu
15. Samaki wanaofugwa kwenye _______ la shule hawaruhusiwi kuvuliwa ovyo.
    a. Leso b. pojo c. fuo d. lambo e. rodi
16. Ili nyama isioze ni vema ihifadhiwe kwenye _____________
    a. Jarife b. nduli c. jokofu d. pantone e. bucha
17. Mhunzi ni kwa chuma na ___________ ni kwa mwenye elimu ya nyota. Neno lipi linakamilisha sentensi hii?
    a. Mnajimu b. sonara c. mwashi d. mhunzi e. mhadhiri
18. Askari kanzu wanaandikiana barua kila siku. Sentensi hii ipo katika kauli gani?
    a. Kutendwa b. kutendeana c. kutendana d. kutenda e. kutendeka
19. Kauli halisi ya sentensi isemayo, Rais alisema kwamba tunatakiwa kutii sheria bila shuruti ni ipi?
    a. "Hamtakiwi kutii sheria"
    b. "Tiini sheria" kama Rais alivyosema
    c. " Sheria zifuatwe" Rais alisema
    d. Rais alisema "Tiini sheria"
    e. "Mnatakiwa kutii sheria bila shuruti," Rais alisema

20. Baada ya mvua kunyesha ulitokea ukungu mwingi. Neno ukungu limetumika kama aina gani ya maneno?
    a. E    B. Ts    c. V    d. t    e. N
21. Mtu anayeandika muhtasari wa mambo yanayojadiliwa mkutanoni huitwa______
    a. Mwenyekiti    b. mhasibu    c. karani    d. mpiga chapa    e. katibu
22. Vizuri vyote vimepelekwa sokoni leo. Neno lipi limetumika kama kivumishi katika sentensi hiyo?
    a. Vyote    b. vizuri    c. leo    d. sokoni    e. vimepelekwa
23. **Huna budi** kuhudhuria darasani kila siku. Maana ya maneno " **huna budi**" maana yake ni _____
    a. Unatekeleza    b. kusudia    c. haikulazimu    d. si lazima    e. inakulazimu
24. Kinyume cha neno uovu ni____
    a. Upole    b. adili    c. uadilifu    d. amani    e. uchapakazi
25. Mwajuma na Rose **ni** watoto wa mjumbe. Neno **<u>ni</u>** limetumika kama
    a. Kiwakilishi    b. kitenzi kisaidizi    c. kitenzi kishirikishi    d. kiunganishi    e. kihusishi
26. Nahau piga mtindi ina maana gani?
    a. Piga makasia    b. chota maziwa    c. mwaga mtindi    d. chota maziwa    e. lewa pombe
27. Mama Chupaki atakula mumbi leo maana anakwenda shambani na mtoto bila kumchukulia maziwa. Nahau **kula mumbi** maana yake ni
    a. Kula vumbi    b. kula uji    c. tembea haraka    d. pata taabu    e. wahi kurudi
28. Kamilisha methali isemayo:___________huleta heshima
    a. Kuvaa vizuri    b. nyota njema    c. kuwahi kazini    d. jina jema    e. mwenda mbio
29. Methali ipi kati ya zifuatazo haitoi onyo juu ya tabia ya mtu?
    a. Kiburi si maugwana
    b. Mkaidi hafaidi mpaka siku ya idi
    c. Penye nia pana njia
    d. Samaki mkunje angali mbichi
    e. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
30. Nyumba yangu ni kubwa lakini mlango mdogo. Jibu la kitendawili hiki ni lipi?
    a. Kaburi    b. kiberiti    c. chupa    d. yai    e. kata
31. Methali gani inafanana na ile isemayo " Nyumba usiyolala hujui hila yake?
    a. Kikulacho ki nguoni mwako
    b. Asiyekuwepo na lake halipo
    c. Adhabu ya kaburi aijuaye maiti
    d. Jogoo wa shamba hawiki mjini
    e. Mimi nyumba ya udongo sihimili vishindo
32. Kujikwaa ni jibu la kitendawili kipi kati ya hivi?
    a. Ajihami bila silaha
    b. Napigwa faini kosa silijui
    c. Pruu mpaka Maka
    d. Hana adabu wala stahaa kwa watu
    e. Amevaa kisura
33. Meneja alifukuzwa kazi baada ya kukutwa akila chauchau. Nahau kula chauchau maana yake ni
    a. Kula chakula    b. kutia chumvi    c. kula mlungula    d. kupokea rushwa    e. kupigana kazini
34. Maana ya methali aungurumapo simba mcheza nani ni ipi?
    a. Mwenye nguvu mpishe
    b. Simba mwenda pole ndiye mla nyama
    c. Ukiona vyaelea ujue vimeundwa
    d. Wema hauozi
    e. Simba ni mnyama mkali
35. Malizia methali hii: mcheka kovu____________
    a. Huchekwa pia    b. hupata madhara    c. hula mema    d. asiyefikwa na jeraha    e. si mzuri

## SEHEMU B: UTUNGAJI

Umepewa sentensi zilizochanganywa zipange katika mtiririko wenye mantiki kwa kuzipaa herufi A, B, C, D na E ili zilete maana

36. Wote humfikiria malkia kuwa ni mkuu na mama yao
37. Watoto wakikua hujiunga katika kazi za kujitegemea katika kijiji chao
38. Ushirikiano wao mwema umewafanya wawe na nguvu sana hivyo huogopwa na viumbe wengi hata wanyama wakubwa
39. Kazi ya kila mmoja hutegemea sana umbo na uwezo wake
40. Wale wenye viwiliwili vikubwa na wenye nguvu huwa askari na wote waliobaki huwa wafanyakazi

## SEHEMU C: USHAIRI

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali**

Ewe ulo na busara, fikiri bibi na bwana
Fikiri lilo tohara, na lile lilo dhamana
Pia, fikiri izara, na ujana una mwisho
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho

Ujana ni jambo bora, ameupamba Rabana
Tena umetia fora, ulitendalo hufana
Basi usiwe mkora, akiba uweke sana
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho

Kuweka jambo dharura, jikimu kuweka mwana
Siyo pato kulipura, kwa usiku na mchana
Ukitoweka ajura, elewa umekubana
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho

Maswali

41. Badala ya kutumia neno Rabana mwandishi angeweza kutumia neno gani?
42. Neno hadaa kama lilivyotumika katika shairi hili lina maana gani?
43. Andika kibwagizo cha shairi hili
44. Vina vya kati katika ubeti wa pili ni vipi?
45. Mwandishi wa shairi hili anatoa wosia kwa nani?